SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.25 NO. 1 2026
DOI: 10.51984/x72wsp42

جامعة سبها للعلوم الإنسانية مجلة
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: http://www.sebhau.edu.ly/journal/johs

# KUCHUNGUZA USEMEZANO KATIKA RIWAYA YA VUTA N'KUVUTE YA SHAFI ADAM SHAFI

*Salama Salem Salama & Mohamed Omary Maguo

Department, Swahili languagethe faculty of arts and social sciences,Open University,Dar es Salaam, Tanzania

**Keywords:**
Usemezano
Riwaya
Vuta N'Kuvute

**Ikisiri**

Makala haya yanaangazia usemezano katika riwaya ya Vuta N'kuvute iliyoandikwa na Shafi Adam Shafi ikiwa ndilo lengo la makala haya. Nadharia ya usemezano ndiyo ambayo imetumika katika kukusanya kuchambua data za utafiti huu kwa kuzingatia vipengele husika vilivyotajwa na Bakhatin (1981). Data za makala haya zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Matokeo ya makala haya ni kwamba, Shafi Adam Shafi katika riwaya yake ya Vuta Nkuvute ametumia vipengele vya usemezano kama mbinu ya kujenga na kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Miongoni mwa vipengele hivyo ni uzungumzi nafsi, majibizano, dhana ya shani, na sajili za lugha.

# دراسة العلاقة في رواية "الشد والجذب" لـ: شافي أدم شافي

*سلامة سالم سلامة و محمد عماري ماقو

قسم اللغويات والدراسات الأدبية، كلية الاداب والعلوم الاجتماعية، الجامعة المفتوحة، دار السلام، تنزانيا.

**الكلمات المفتاحية:**
العلاقة
رواية
الشد والجذب

**الملخص**

تسلط هذه المقالة الضوء على استخدام الجداول في رواية فوتا نكوفوتي للكاتب شافي آدم شافي، والتي تشكل محور هذه المقالة. وقد تم استخدام نظرية الخطاب في جمع وتحليل البيانات لهذه الدراسة، مع الاهتمام بشكل خاص بالجوانب المهمة التي ذكرها باختين (1981). تم جمع البيانات الخاصة بهذه المقالة باستخدام نهج القراءة المتأنية وتم تحليلها باستخدام التحليل الوصفي. خلاصة هذه المقالة هي أن شافي آدم شافي، في روايته فوتا نكوفوتي، استخدم عناصر البلاغة كأسلوب لبناء رسالة ونقلها إلى جمهوره. إذا كنت لا تعرف ماذا تفعل، فلن تحتاج إلى القلق بشأن ذلك، ولن تشعر بالقلق بشأن ذلك. وقد ساهمت هذه العناصر بشكل كبير في تصوير السياق الاجتماعي والسياسي والثقافي في ذلك الوقت. من يستخدم الميزانو، فقد تمكن المؤلف من استحضار الصراعات الطبقية والتواصل بين الشخصيات المختلفة. علاوة على ذلك فإن اللغة المستخدمة تعكس واقع المجتمع في ذلك الوقت.

## 1.0 Utangulizi

Katika riwaya, usemezano huonekana hasa pale mtunzi anapowachora wahusika wakiwa katika maongezi ya kawaida au wakizungumza faraghani. Jambo hili limethibitishwa na watafati mbalimbali. Suiter (2017), amethibitisha uwepo wa usemezano katika ushairi kupitia Diwani *ya Sikate Tamaa* na kubaini kwamba, usemezano upo katika ushairi wa Kiswahili kama ilivyotokea kwa Njogu (1993) ambaye alifanya utafiti na kudhihirisha usemezano katika ushairi wa Al-Inkishafi kinyume na madai ya Bakhtin (1981) kwamba usemezano upo katika riwaya pekee. Matumizi ya usemezano katika Tamthiliya ya Kiswahili, yamethibitishwa pia katika *Mashetani* na *Pambo*.

Kutokana na mawasilisho haya ya kazi tangulizi, tafiti za awali zilijikita hasa katika kuthibisha uwepo wa usemezano katika ushairi, semi, tamthiliya, nyimbo na kadhalika. Hivyo basi, utafiti huu umenuia kuchunguza jinsi vipengele vya usemezano vinavyodhihirika katika riwaya za *Kasri ya Mwinyi Fuad*, *Haini*, *Kuli*, *Vuta N'kuvute* na *Mbali na Nyumbani* za Shafi Adam Shafi (1999) na jinsi vipengele hivi vitakavyofanikisha dhamira na maudhui. Utafiti utachunguza vipengele kumi na tatu kama vilivyoainishwa na Suter (2017) ambavyo ni: uzungumzi nafsia, utendaji, majibizano kati ya wahusika wawili au vikundi viwili, uwingi lugha, dhana ya shani, kronotopu, kuwa na kani pewa na kani kitovu, kanivali, kumiliki sajili nyingi za lugha, lugha ya wahusika, tamko kuwa jibu la tamko, uhusiano na matini zingine na usimulizi wa kisanaa. Vilevile, itachunguza namna vipengele hivi vya usemezano vinamwezesha msomaji kuelewa au kufahamu kile kinacho wasilishwa na mwandishi au mtunzi wa kazi ya sanaa. Hili linazingatia umuhimu wa usemezano katika kufanikisha mawasiliano katika riwaya ya Kiswahili pamoja na jinsi vipengele vya usemezano vinavyoweza kumwezesha msomaji kuelewa au kufahamu kile kinacho wasilishwa na mwandishi au mtunzi wa kazi ya sanaa.

*Corresponding author:
E-mail addresses: salama_2072@yahoo.com ,(M. O. Maguo)Omarymohamed36@out.ac.tz
*Article History : Received 23 April 2025 - Received in revised form 07 December 2025 - Accepted 14 January 2026*

Hii ni kusema, makala haya yataongeza maarifa kuhusu maendeleo ya usemezano katika riwaya ya Kiswahili kwa kurejelea

2.0 Nadharia ya Usemezano

Makala haya yameongizwa na nadharia ya Usemezano ambapo Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa, usemezano ni dhana ambayo inatokana na Kiarifa "kusemezana." Istilahi hii ilitumika kabla ya "Usemezano" kuundwa. Nadharia hii imeundwa na vipengele vifuatavyo:

**(i) Uzungumzi Nafsia**

Uzungomzi nafsia ni namna moja ya usemezano (Mulokozi, 1996). Hii ni kutokana na mtu kuzungumza na nafsi yake. Bakari (2008) amejadili namna ambavyo watunzi wa karne ya 20 wameathiriwa na Muyaka.

**(ii)Tamko ni Jibu la Tamko Jingine**

Hapa usemezano hudhihirika hasa pale ambapo watunzi wa kazi za sanaa wanaposemezana kwa kupitia tungo zao. Yaani utungo kuwa jibu kwa utungo mwingine kama asemavyo Bakhtin kuwa, tamko ni jibu kwa tamko jinguine.

**(iii) Utendaji**

Utendaji ni namna au jinsi ya kufanya jambo. Hiki ni kipengele cha usemezano ambacho kinaruhusu utagusano wa kisemezano. Katika mjadala, lazima mtunzi wa kazi za sanaa ajitambulishe kwa hadhira yake. Bakhtin (1986) anaeleza kuwa, utendaji ni mbinu mojawapo ya lugha na ni namna ya kuzungumza.

**(**iv) Majibizano

Majibizano ni hali ambayo mtu au kundi la watu wanaotupiana maswali na majibu.

**(v) Usimulizi wa Kisanaa**

Wamitila (2002) anasema kwamba, usimulizi ni utambaji au maelezo ya jambo fulani. Usimulizi unatazamwa sambamba na kipengele cha wakati. Katika usimulizi sauti ni muhimu sana kwa sababu huonyesha ya kwamba hadithi imesimuliwa kwa nafsi ya kwanza, ya pili naya tatu. Vilevile katika usimulizi, msimulizi na msimuliwa husikiliza kwa umakini.

**(vi) Uwingi Sauti**

Kazi za riwaya huonyesha sauti tofauti ambazo zipo huru na hazifungwi na sehemu yoyote. Sauti haiwezi kurejelea msemaji peke yake bali pia hurejelea yale mahusiano ya nguvu yanayoathiri na kumweka msomaji katika hali Fulani.

**(vii) Sajili Mbalimbali**

Kazi za fasihi hutumia sajili mbalimbali ili kurahisisha uwasilishaji wa ujumbe. Baadhi ya sajili hizi ni magazeti, sajili ya sharia, mazungumzo, biashara kama ilivyo katika riwaya *ya Vuta n'kuvute* mzee Raza mme wake Yasmini alikuwa akifanya biashara ya duka Zanzibar na Mombasa.

**(viii) Kronotopu**

Wamitila (2002) anasema kuwa, kronotopu ni matukio yanayotokea hasa katika mpito wa wakati na mahali Fulani. Kronotopu kimsingi hurejelea hali ya kazi za kifasihi zinazoweza kukiuka mipaka ya mahali na wakati kiasi cha kutoweza kuonekana kwamba, kazi Fulani ya riwaya ya ni kipindi gani au wakati gani. Mfano ni kazi kama ya Bina-Adam ambayo inaakisi wakati wa kidhahania, usioeleweka kuwa na athari za kisaikolojia.

**(ix) Kuwa na Kani Pewa na Kani Kitovu**

Wamitila (2002) akimrejelea Bakhtin (1981) kani pewa ni sifa ya utanzu Fulani au mtindo ambao unaweza kubadilika katika mpito wa wakati huku kani kitovu na ni sifa ya utanzu ambao haubadiliki. Kuna utofauti baina ya kani pewa na kani kitovu. Utofauti huu unaleta upinzani ambao unatenganishwa na kani kitovu iletayo mshikamano katika masimulizi au maandishi.

**(x) Kanivali**

Ntarangwi (2004) anasema kuwa, kipengele cha kanivali ni muhimu katika uhakiki wa Bakhtin kwa sababu husaidia kubainisha usemezano katika kazi za fasihi.

Kupitia nadharia hii tumeweza kubainisha vipengele vya usemezano katika riwaya ya Vuta N'kuvute na kutimiza lengo la makala yetu.

3.0 Mbinu za utafiti

Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini ambayo ni mbinu ya kukusanya data kwa kusoma kwa makini matini husika kwa kufuata hatua maalumu zinazowezesha kupatikana kwa data za utafiti (Kothari, 2004; Kumar, 1999). Hatua hizo ni pamoja na kusoma matini husika kwa mara ya kwanza bila kudondoa, hatua ya pili ni kusoma na kuanza kudondoa sehemu zinazohusiana na malengo ya makala na kuziweka kwenye daftari maalumu la kukusanyia data, hatua ya tatu ni kuzipanga data zinazofanana na kutenganisha zinazotofautiana na hatua ya nne ni kuziweka data kwenye mpango rahisi wa kuzichambua. Baada ya kukusanya data zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo.

4.0 Usemezano katika *Vuta N'kuvute*

Katika sehemu hii tumewasilisha vipengele vya usemezano kutoka katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* kama ifuatavyo:

4.1 Uzungumzi Nafsi

Uzungumzi nafsi ni namna mtu anavyozungumza na nafsi yake kuhusu masuala yanayokuwa yana mtatiza. Pia, mgogoro wa nafsi ambao mhusika huwa anazungumza na nafsi yake kwa lengo la kutafuta namna ya kuutatua. Bakari (2008) anaeleza kuwa uzungumzi nafsi ni njia mojawapo ya usemezano. Hali hii inatokana na mtu kuzungumza na nafsi yake. Mulokozi (1996) amezungumzia namna baadhi ya watunzi wa karne ya ishirini walivyoathiriwa na utunzi wa Muyaka katika Shairi la "*Moyo*." Msemaji ni moyo wake na msemezwa ni nafsi yake. Moyo unamwambia msemewa kufanya jambo kwanza, lakini asifanye ishara. Shairi hilo linachora tofauti kati ya kile moyo unasema na kile nafsi inatamani.

Mtunzi wa riwaya ya *Vuta N'kuvute* katika kipengele hiki cha uzungumzi nafsia amekidhirisha kupitia wahusika wake, kama alivyomuonesha Yasmin alivyokuwa akiwaza na kuzungumza na nafsi yake kuhusu alivyoathirika na kitendo cha kuozeshwa na mume asiyemtaka yaani mume asiye chaguo lake na namna alivyochukua uamuzi wa kuachana na mume wake na hivyo kuwaza atakavyo kwenda kwa wazazi wake akijua amevunja makubaliano na matakwa yao. Shafi anasema:

> "Aliwaza na kujiuliza, Nende kwa mama?" alifikiria, Aa, nikienda huko mambo yatakuwa mabaya zaidi." (uk. 17).

Vile vile, mtunzi anaonesha kuwa Yasmin baada ya kuamua kumtoroka mume wake Mombasa, aliwaza na kufikiri atakavyowaeleza wazazi wake. Hivyo, njia nzima alikuwa akizungumza na nafsi yake kuhusu wazazi wake watakavyolipokea suala hilo. Mtunzi anaeleza:

> "Njia nzima yasmin kichwa kilikuwa kikimduru akifikiri hali ya uadui atakayokwenda kupambana nayo kwa mama yake. Alikwenda akiwaza atamjibu nini bimkubwa yule atakapoanza kumwuliza maswali. Wakati yumo katika mawazo hayo, alijistukia amekwishafika Kiponda amesimama mbele ya mlango wa nyumba ya mama yake, akijiuliza. "Niingiye au nisiingiye?" (uk. 42).

Uzungumzi nafsi mwingine unajitokeza, hasa pale Yasmin alivyokuwa akizungumza na nafsi yake kuhusu mapenzi. Mtunzi anatuonyesha jinsi Yasmin alivyompenda Denge kupitiliza ilhali Denge mwenyewe alikuwa hapendeki. Denge mapenzi yake aliyaelekeza katika harakati za kutafuta uhuru. Vile vile, Shihabu naye alimpenda Yasmin kupindukia mpaka wivu ukamsababishia kifo. Shafi anasema:

> "Na mtu mwenyewe wa kukoroga hiyo miti shamba ni nani hasa?" Denge?" alijiuliza Yasmin. "Mtu mwenyewe hata wakati wa kujiangalia mwenyewe hana."…..Akamfikiria Shihabu mume wake aliyempenda, akamtunza, akamwonea wivu ukataka kumtia wazimu."Ah! Mungu amrehemu!" Aliomba Yasmin. Akili yake ilikuwa katika mzunguko wa mawazo, yote yamejitokeza mbele ya macho yake kama ndoto." (uk. 246-247).

Uzungumzi nafsi mwingine umejidhihirisha pale Yasmini alipofukuzwa na wazazi wake na hivyo kwenda kuishi na Mwajuma ambaye alikuwa ni maskini hana kitu, lakini alikubali kumpokea Yasmin na kuishi naye. Hivyo, Yasmin aliwaza na

kuzungumza na nafsi yake. Mwandishi anasema:

> "Yasmini sasa hakuwa na mwingine wa kumtegemea isipokuwa Mwajuma, lakini mpaka lini ataendelea kumtegemea? Alijiuliza. Mwanamke mwenzake, mjane kama yeye, hana mbele wala nyuma. "Ah, haidhuru nitaishi hivyohivyo, yache maji yafuate mkondo na upepo, uvume utakapo kwani wangapi duniani wenye dhiki. Mwisho wa dhiki si dhiki, ni faraja tu," Yasmini alijipa moyo" (uk. 43).

Vile vile, Yasmin aliendelea kuzungumza na nafsi yake kama mtuzi anavyobainisha. Mtunzi anasema:

> "Haidhuru, matatizo ndiyo maisha yenyewe, bila ya matatizo hakuna maisha. Matatizo mengi nimekwishapambana nayo, mengine bado naendelea kupambana nayo. Haya ya sasa wacha yawe pamoja na yale nnayopambana nayo" ( uk. 145-146).

Katika dondoo hizo, mtunzi amebainisha uzungumzi nafsi kupitia Yasmin alivyokuwa akisemezana na moyo wake kuhusu watu walivyokuwa wakimpenda, na namna mpenzi wake aliyepoteza maisha kutokana na wivu. Pia, alimpenda Denge kupindukia, lakini yeye Denge alikuwa hana kitu. Alimpenda kwa dhati kutoka moyoni mwake hadi akahisi huenda Denge kamkorogea mitishamba. Hivyo, uzungumzi nafsi umedhihirika kwa kiasi kikubwa katika riwaya hii.

4.2 Majibizano

Majibizano ni hali ambayo watu zaidi ya mmoja au vikundi viwili vinabadilishana usemi katika hali ya kubishana hatimaye wanakuwa na makubaliano. Pia, ni njia inayotumika kuwasilisha ujumbe kutoka pande mbili tofauti katika njia ya mmoja kusema na mwingine kujibu au kuongelea kile kilichosemwa. Dhana ya majibizano ni nyeti na mara nyingi huishia kuwakanganya watumiaji wake ambao hutokana na dhana ya majadiliano huwa na uhusiano. Bakhtin (1981 & 1984) anaongelea dhana ya majibizano kama inavyojitokeza katika riwaya na kuanisha aina za majibizano. Kwanza, kuna majibizano kati ya wahusika wawili au zaidi wanaozungumza kama ilivyo katika maongezi ya kawaida.

Pili, usemi mmoja hufumbata sauti za watu wawili tofauti. Hii ni kuwa usemi huo unaweza ukawa jawabu kwa semi zilizotangulia na zitakazofuata. Pamoja na kuwepo uchangamano huu, aina hizi za majadiliano kama zilivyozungumziwa na Bakhtin zimeweza kueleweka na kuzingatiwa katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*. Kipengele hiki kimefafanuliwa kwa undani na kuonesha namna usemezano ulivyojitokeza kutokana na mtunzi kutumia wahusika kusemezana kupitia majibizano yanayoonesha wahusika kulumbana kama anavyodhihirisha mtunzi:

> "Usinikere Bwana mimi nataka kulala.""Mbona unalala mapema? N'do kwanza saa mbili. Amka tuzungumze, "Bwana Raza aliunguruma. Yasmin alipuuza akalala."(uk. 03).

Vile vile majibizano yamebainishwa kwa kuonesha malumbano ya Yasmin na mumewe Mzee Raza kuhusu kuhamia Mombasa baada ya shughuli ya biashara kudorora Unguja. Suala hilo Yasmini hakulifurahia, majibizano yalijitokeza kama mtunzi anavyobainisha:

> "Tukafanye nini?"
> "Kwani sikukwambia?"
> "Kitu gani?"
> "Kwamba mjomba amenijibu ile barua yangu."
> "Aa mimi hukuniambia."
> "Ala! Basi labda nimesahau, mjomba amenijibu ile barua niliyompelekea na amenishauri kuhamia Mombasa nikafanye biashara ya mboga.",,,,,,,"Bwana Raza alimuuliza mkewe, "Unasemaje?" Yasmin alijibu, "Ah! Haya maisha tunoishi mimi na wewe, mimi yashanitumbukia nyongo. Mimi nahisi bora unipeleke kwetu wakati utakapokwenda Mombasa." (uk. 01).

Mtunzi anasema:


> "Tukafanye nini?"
> "Kwani sikukwambia?"
> "Kitu gani?"
> "Kwamba mjomba amenijibu ile barua yangu."
> "Aa mimi hukuniambia."
> "Ala! Basi labda nimesahau, mjomba amenijibu ile barua niliyompelekea na amenishauri kuhamia Mombasa nikafanye biashara ya mboga.",,,,,,," Bwana Raza alimuuliza mkewe, "Unasemaje?" Yasmin alijibu, "Ah! Haya maisha tunoishi mimi na wewe, mimi yashanitumbukia nyongo.Mimi nahisi bora unipeleke kwetu wakati utakapokwenda Mombasa." (Shafi, 1999:01).


Pia, kuna majibizano kati ya Mwajuma na Kachero baada ya Denge kuondoka nyumbani kwa Mwajuma. Kkachero anayemfuatilia Denge na kundi lake naye alifika kwa Mwajuma akimwulizia Denge. Mwandishi anaeleza:

> "Unamjua Denge?" aliuliza yYule askari kanzu.
> "Namjua" alijibu Mwajuma mbiyo mbiyo.
> "Unamjua vipi?"
> "Namjua tu, hivyo hivyo, hujambo sijambo, basi, hakuna zaidi" Mwajuma alijibu, wasiwasi umemjaa akiona sasa Denge amzulia balaa labda kwa yale makaratasi yake.
> "Kwani kafanya nini?
> "Sikiliza dada," alisema askari kwa sauti ya upole. Mimi sikuja hapa kwa dhamira mbaya ila nataka kuomba msaada wako. Denge ni mtu mbaya na sisi tunamtafuta, nafikiri wewe utaweza kutupa habari zake."
> "Ubaya wake nini?"
>
> "Denge ni Koministi, kasoma Urusi na watu wa namna hiyo ni hatari sana. Watu wa namna hiyo hawaamini Mungu, tena wanataka kuleta fujo kubwa nchini."
> "Sasa nisikilize," alianza yYule askari, "mimi nataka ufanye jambo moja"
>
> "Jambo gani?" Mwajuma aliuliza.
> "Mimi nataka Denge anapokuja hapa umsikilize maneno yake vizuri, usikilize nini anasema, nani

> rafiki zake anaofuatana nao, nini anataka na kila analosema umsikilize kwa makini halafu yote atakayoyasema uje uniambie nitakapokuja tena". (uk. 64-65).

Katika dondoo hii, mtunzi ametumia usemezano kupitia kipengele cha majibizano kama alivyothibitisha mafungu hayo. Usememzano ni nguzo ya msingi katika kufanikisha kazi inayohusika.

4.3 Dhana ya Shani kwa Msingi wa Bakhtin

Shani ni kipengele cha usemezano kilichoasisiwa na Bakhtin (1981). Shani ni jambo linaloshangaza na ambalo si kawaida yake kutokea kwani linastaajabisha. Shani ni vituko, mambo yanayokera au kuudhi. Mfano ni pale watu wanapomwamini mtu na kumpa uongozi au madaraka, lakini mtu huyo au watu hao wakatumia vibaya madaraka hayo. Mtunzi anasema:

> Kama hukuweza kuishi na Raza, basi na sisi hatuna pa kukuweka" mjomba wake Yasmin alisema kwa kelele. Kelele zilikuwa kubwa mpaka majirani wakaanza kuchungulia madirishani. "Tena upesi tuondokee mbele ya macho yetu utafute pa kwenda. Toka!" alifoka mjomba…..Yasmin akamjibu mjomba wake, "Niondoke nende wapi na hapa ndiyo kwetu?"
> "Hapa palikwa kwenu kabla ya kuolewa. Sisi tulikupa mume ili tupungukiwe na mzigo. Sasa kwa kuwa umemkimbia mumeo, tafuta pa kwenda." Yasmin mabega yalimporomoka, asijue la kufanya. Alitoka nje taratibu na alipofika nje mjomba wake aliufunga mlango kwa nguvu huku akilaani na kutukana"(uk. 18-19).

Vile vile, Yasmini alipo kwenda kwa mama yake naye alimfukuza. Hakutaka kabisa kumuona pale nyumbani. Mtunzi anasema:

> "Umekujisha kufenza nini hapa wewe mwenaharamu, umeacha Raza Mombasa umekujisha Zanzibar kufenza uhuni kutilisa sisi aibu. Jamatini vatu ote nazungumza habari yako, nasema veve siku hizi nafatana na golo. Toka! Toka kwenda zako! Mimi sitaki ona hata uso yako. Kuranjiso, kama veve nakuja tena hapa mimi taita askari, tasema veve miji nataka iba. Muhuni ve, mwenaharamu, toka!"(uk. 42-43).

Dondoo hizo ni shani kwani kitendo cha kumtolea mtoto wao lugha za matusi kwa kosa la kumkataa mume waliomtaka wao ni kitendo kisichokubalika katika jamii zetu. Kupitia kipengele hiki, Shafi ametumia kipengele hiki cha shani kuonesha au kufungua macho wanajamii ili kukashifu uongozi mbaya katika jamii za kitanzania na Afrika kwa ujumla.

4.4 Sajili za Lugha

Sajili ni muktadha au mitindo maalumu ya lugha inayojitokeza katika hali au mazingira tofauti katika jamii. Mifano ya sajili ni kama vile lugha ya hospitalini, shuleni, sajili ya dini, biashara, barua, siasa na michezo. Kila sajili huwa na sifa mbalimbali zinazoitofautisha sajili hiyo na nyinginezo. Sajili huambatana na aina ya mahusiano walionao wazungumzaji, sehemu yanakopatikana mazungumzo hayo, lengo la mazungumzo hayo, mazungumzo hayo ni baina ya nani na nani, na istilahi zinazopatikana katika mazingira yanakofanyika mazungumzo hayo (Mwalimu wa Kiswahili, 2020). Kazi za fasihi hutumia sajili mbalimbali ili kurahisisha uwasilishaji wa ujumbe. Katika matumizi ya sajili tofauti ndipo usemezano huweza kupatikana katika matini. Baadhi ya sajili zilizojitokeza katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* zimeelezwa katika sehemu hii.

4.4.1 Sajili ya Biashara

Katika sajili ya biashara, usemezano unajitokeza kutokana na watu wawili kusemezana au kubadilishana usemi, yaani mtoaji na mpokeaji bidhaa. Kuna mnunuzi na muuzaji. Biashara ya kuuza bidhaa kama anavyoeleza mtunzi wa riwaya ya *Vuta n'kuvute*. Anaeleza:

> "…Mwuza kahawa alikuwa kazungukwa na washititi wake….wauza mandazi na samaki wa kukaanga wamejipanga nje ya ule mkahawa, sinia zao zimejaa. Walikuwa watoto wa kike na wa kiume, wapo pale kutabaruku wapate pesa mbili tatu za kusaidia nyumbani" (uk. 94).

Vile vile, shughuli ya biashara mtunzi ameionyesha pale wakina Yasmin na Mwajuma walipokwenda kufanya manunuzi ya vipodozi na manukato na vitambaa vya bei kubwa katika maduka makubwa. Shafi anasema:

> "Yasmin na Mwajuma walikuwa ni kuingia duka hili na lile. Tena siyo maduka ya Mchangani na Darajani ambayo yalikuwa maarufu kwa vitambaa vyake vya mkono shilingi, la waliingia ndani ya maduka ya Shangani na Banghani;maduka ambayo wanunuzi wake walikuwa ni akina el-nani na el-nini. Shilingi mia sita zilikuwa zikimwasha, na alitaka kumdhibitishia shoga yake aliyemfadhili siku nyingi kwamba naye si miongoni mwa wale waliokuwa watovu wa fadhila wasiokuwa na ihsani. Madukani mle walipigana vikumbo na akina mabibiye ambao kila mmoja alijiona hakuna tena kama yeye. Afadhali Yasmin, wao walifikiri ni bibiye kama wao, lakini walipomwangalia Mwajuma walimwona kama kisonoko tu kilichotumwa kumsindikiza bibiye mwenzao madukani." (uk. 126).

Katika sajili ya biashara mtunzi ameitumia ili kukuza mawasiliano kwa wahusika wake. Kitendo cha muuza bidhaa na mnunuzi ni usemezano kwani tunaona pande mbili zinawasiliana na kusikilizana. Kitendo hicho kinadhihirishia kuwa katika sajili ya biashara usemezano lazima uwepo kutokana na mazungumzo au majibizano ya watu wawili.

**4.4.2 Sajili ya Siasa**

Mtunzi wa riwaya ya *Vuta n' kuvute* ametumia sajili ya siasa kutokana na mvutano uliopo kati ya makundi mawili yaani watawala na watawaliwa. Kundi la wanaodai haki yaani kundi la wakina Denge na Wazungu, yaani watawala, ambao wanapambana na wanaotafuta ukombozi. Sajili hii inadhihirika pale ambapo kuna mvutano wa kisiasa kati ya makundi mawili yaani watawala na watawaliwa. Wazungu na Waswahili, kundi la akina Denge ambao wanapambana na kuvutana katika kutafuta uhuru wao. Wakoloni wanawasaka akina Denge ili kusitisha harakati zao za kudai uhuru. Misamiati ya kisiasa inayoonekana hapa ni komunisti, bwata, ukoloni, wanasiasa, uhuru, mapambano, majukwaa, utawala mtunzi

amedhihirisha mvutano huo. Shafi anasem:

> "…..Inspekta Wright alisheherekea ushindi wake English Club kwa kunywa pombe, akijisifu na kujigamba mbele ya wenzake kama kwamba amefanikiwa kweli kulizuia wimbi la mapambano ya kupigania uhuru visiwani Zanzibar. Lakini sivyo kabisa, kufungwa kwa Denge na Chande kulikuwa kama cheche iliyosababisha moto mbugani. Wana siasa walipiga kelele majukwaani, wananchi wakalaani ukoloni."(uk. 227).

Mtunzi anaendelea kusema:

> "…...You don't know? Hapana jua wewe nafanya nini?" Alibwata Kamishna matusi yakaanza kumtoka. Alimsumbulia na kumsimanga Denge jinsi alivyokuwa hana shukrani kwa utawala wa Kiingereza kwa ustaarabu waliowafundisha watu wa Zanzibar.,,,,,"
> Alimsihi Denge asishirikiane na watu wabaya, akamtahadharisha kwamba polisi wanamwangalia kwa macho mawili na wanazijua nyendo zake zote. Alimwomba atulie na kumwahidi cheo kikubwa pindi akifanya hivyo. Alimlaghai na kumpaka mafuta kwa mgongo wa chupa na alipomamaliza akamwambia, "Now go, you are free." "I wish I were!" alimjibu, akanyanyuka na kwenda zake bila ya hata kugeuka nyuma…" (uk. 204).

Katika dondoo hizi, tumeona mtunzi alivyobainisha sajili ya siasa na namna siasa hizo zilivyokuwa ni za kuwakandamiza wanyonge waliokuwa wakipambana kwa lengo la kutaka uhuru wao.

4.4.3 Sajili ya Mazungumzo

Sajili ya mazungumzo ni aina nyingine ya kipengele cha usemezano kilichotumiwa na mtunzi Shafi Adam. Mazungumzo hupatikana pale wahusika wawili wanapo wasiliana kwa kupokezana na kuweza kupashana habari. Katika sajili ya mazungumzo, tumeangalia namna mtunzi alivyotumia mazungumzo ili kufikisha ujumbe wake kwa hadhira kupitia wahusika wake waliokuwa wanazungumza mazungumzo. Kuna mazungumzo ya Yasmini na mke wa mjomba wake baada ya kutoka Mombasa alipomtoroka mume wake bwana Raza. Shafi anasema:

> "Mjomba yupo? Aliuliza Yasmin hata bila ya kusalimu.
> Hayupo, kenda Jamatini. Mbona ghafla? Habari za Mombasa?"
> "Mbaya."
> "Kwa nini?"
> "Kwanza usiniulize maswali mengi, njaa imenishika tena nimechoka, kama kipo chakula nigaiye kwanza nile halafu tutazungumza" (uk. 17).

Mazungumzo mengine ni kati ya Yasmini na Mwajuma baada ya Yasmin kufukuzwa na mjomba wake na kwenda kwa Mwajuma ili amsaidie na kumsitiri. Mtunzi anasema:

> "….. Yalikuwaje shoga yangu?"
> "Ah, mambo makubwa, hata sijui nikwambie nini. "Karibu jikoni basi tupike." Mwajuma alimsogezea Yasmin mbuzi na kumkaribisha akae yeye mwenyewe akiendelea na mapishi. "Enhe! Khabari za Mombasa?"
>
> "Khabari shoga yangu mbaya, Maisha na Bwana mkubwa yule yamenishinda. Sina raha sina starehe, mwisho nimeona bora nirejee kwetu kwa wazee wangu. Nimekwenda kwa mjomba wangu nimetimuliwa kama mbuzi na kwa mama naogopa kwenda manake maneno yake nayajua." Yasmini, " Sasa hata sijui la kufanya usiku huu," aliendelea huku akiweka kikapu chake ,".Maskini shoga yangu, sasa una shauri gani?" Mwajuma aliuliza kwa huruma za dhati. "Sina shauri lolote, nimekuja kwako kukusikiliza utaniambia nini. Tafadharinisitiri, nisitiri aibu yangu!"
>
> Mwajuma alimtazama Yasmin akatikisa kichwa. "Basi karibu shoga, tutajibana hapa hivyohivyo, ijapokuwa kitanda chenyewe ni kimoja," alimwambia na kumwongoza chumbani akipangusa mikono kwa kanga aliyojifunga kifuani. (uk. 19-20).

Vile vile, mtunzi anawatumia Mwajuma na Yasmin wanaomzungumzia Denge kutokuwa na kitu, yaani ni maskini ingawa katoka Ulaya. Mtunzi anasema:

> "…Mbona anaonekana msharimshari hivi?"
>
> "Ah, hana chochote, kila ukimwona n'do Vile vile,, kutwa anaranda tu. Kila ukimwona kabeba magazeti na makaratasi mkononi, tena karejea Ulaya hivi karibuni"
>
> "Ulaya?" Yasmin aliuliza kwa kustaajabu macho ameyatumbua.
> "Wewe huzioni hizo mbwembwe zake?"
>
> "Basi mtu mkubwa." Yasmin ameshangaa utafikiri kaambiwa mtu Yule katoka mbinguni.
>
> "Mtu mkubwa gani, nakwambia kazi yake kuranda tu, hafanyi kazi yoyote."
> "Itakuwaje, iwe katoka Ulaya halafu hana kazi?" Yasmin alibisha. (uk. 48-49).

Katika dondoo tulizozibainisha, kipengele hiki cha mazungumzo kimedhihirika katika riwaya hii ya *Vuta N'kuvute,* kupitia mazungumzo usemezano unapatikana kutokana kuwepo kwa mazungumzo ya watu wawili au zaidi kusemezana na huo ndio usemezano.

5.0 Hitimisho

Katika makala haya tumeshughulikia vipengele vinne vya usemezano ambavyo ni uzungumzi nafsi, majibizano, dhana ya shani na sajili za lugha. Kupitia vipengele hivi tumeweza kuona namna ambavyo mtunzi wa riwaya ya Vuta N'kuvute anavyotumia mbinu ya usemezano katika utunzi wa riwaya hii na kuwezesha kuwasilisha

ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Matumizi haya ya mbinu ya usemezano yanamfanya mtunzi Shafi Adam Shafi kuwa na upekee katika riwaya zake.

MAREJELEO

Bakari, M. (2008). Usemezano kama mkakati wa kufahamu riwaya za *Babu Alipofufuka*, *Bina-Adamu* na *Mkusanyiko wa Hadithi fupi*. Shahada ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kothari, C. R. (2004). *Reseach Methodology: Methods and Techiniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Kumar, R. (1999), Reserch Methodology Astep by guide for beginners. SAGE Publication. New Delhi.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.

Mwanzandi, I. (2002). *Usemezano katika Umalenga wa Kiswahili*. Shahada ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Egerton.

Njogu, K. (1993). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi University Press.

Njogu, K., & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ntarangwa, M. (2004). *Uhakiki kazi za Fasihi.* Augustana College: Rock Island.

Shafi. A. S. (1999). *Vuta n'kuvute.* Dar-es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers Ltd

Suter, D. (2017). Usemezano katika Diwani ya Sikate Tamaa; Tasinifu ya Uzamili chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi na Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi Phonix Publishers Ltd.

Mwalimu wa Kiswahili (2020). Sajili katika Isimu Jamii.mwalimuwakiswahili.co.tz